



TANGAZO LA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI WA ELIMU YA AWALI SHULE YA MSINGI
YA MCHEPUO WA KIINGEREZA NYASA

(NYASA ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL)

Shule ya Msingi Nyasa (Nyasa English Medium Primary School) ilianzishwa na kuendeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ili kukidhi hitaji la wananchi wa Wilaya ya Kyela ya kuwa na Shule ya Mchepuo wa Kiingereza. Shule hii haipokei fedha za ruzuku ya uendeshaji kutoka serikalini hivyo inaendeshwa kwa kupitia **ada na michango mingine** ya **wazazi**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anatarajia kufanya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la Elimu ya Awali (Pre-Primary) katika shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza Nyasa (Nyasa English Medium Primary School) siku ya Alhamis **15 Desemba, 2022**.

Uandikishaji huo unatarajiwa kuanza saa **4 Asubuhi** hivyo wazazi wote kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela wenye watoto wa kuanzia umri wa miaka **4 $\frac{1}{2}$** hadi **5 $\frac{1}{2}$** wanatangaziwa kufika shulenii Nyasa tarehe tajwa kwa ajili ya uandikishaji. Aidha wazazi wanatakiwa kuambatana na watoto wao kwa sababu kutakuwa na mahojiano (Interview) mafupi.

Mambo ya kuzingatia siku hiyo:

1. Mtoto aje na mzazi wake.
2. Mtoto awe na umri wa miaka $4\frac{1}{2}$ hadi $5\frac{1}{2}$.
3. Mzazi wa mtoto awe ni mkazi wa Kyela.
4. Fika na cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) cha mtoto.
5. Muda wa kuanza zoezi ni saa 4 Asubuhi.
6. Zoezi hilo litafanyika kwa siku 1 tu.
7. Nafasi zilizopo ni kwa wanafunzi 120 tu.

Limetolewa na:

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KYELA



Ezekiel H. Magehema

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KYELA



OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

MPAKANI ENGLISH MEDIUM PRE & PRIMARY SCHOOL

USAJILI WA SHULE: EM.19679



TANGAZO LA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI WA ELIMU YA AWALI 2023

SHULE YA MSINGI MPAKANI (MPAKANI ENGLISH MEDIUM PRE & PRIMARY SCHOOL) NI SHULE MPYA YA MCHEPUO WA KINGEREZA, IMEANZISHWA NA INAENDESHWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA ILI KUKIDHI HITAJI LA WANANCHI LA KUWA NA SHULE NYINGINE YA MCHEPUO WA KINGEREZA.

SHULE IPO WILAYA YA KYELA KATA YA NJISI BORDER KITONGOJI CHA KILAMBO. SHULE HII HAPOKEI FEDHA YA RUZUKU YA UENDESHAJI KUTOKA SERIKALINI HIVYO INAENDESHWA KWAKUPITIA ADA NA MICHANGO MINGINE YA WAZAZI.

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA ANAWATANGAZIA WANANCHI WA WILAYA YA KYELA KUWA KUTAKUWA NA USAMILI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA DARASA LA AWALI KWA MWAKA WA MASOMO 2023 KATIKA SHULE MPYA YA MCHEPUO WA KINGEREZA MPAKANI YENYE NAMBA YA USAJILI E.M 19679 SIKU YA ALHAMISI TAREHE **8 DESEMBA, 2022**.

FOMU ZA MAOMBI YA KUSHIRIKI ZOEZI HILO ZINAPATIKANA SHULE YA MSINGI MPAKANI ENGLISH MEDIUM KUANZIA TAREHE 01/12/2022 HADI TAREHE 07/12/2022 SAA 1:30 ASUBUHI HADI SAA 11:30 JIONI

MAMBO YA KUZINGATIA

1. MWANAFUNZI WA AWALI AWE NA UMRI KUANZI MIAKA 4 HADI $5\frac{1}{2}$.
2. FOMU YA KUTHIBITISHA KUSHIRIKI IAMBATANISHWE NA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA.
3. PICHA MOJA YA PASSPORTSIZE YA MWANAFUNZI.
4. MUDA WA KUANZA USAMILI (INTERVIEW) SAA 4:00 ASUBUHI.
5. USIKIAPO TANGAZO HILI MTAARIFU NAMWINGINE.
6. NAFASI ZILIZOPO NI KWA WANAFUNZI 100 TU.

Limetolewa na:

Ezekiel H. Magehema

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI WILAYA
KYELA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

KYELA